MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI-TASAF III

1. Utangulizi

Awamu ya Tatu ya TASAF ilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 15 Agosti 2012 mjini Dodoma. Wakati wa uzinduzi, Mhe. Rais alionyesha kuridhishwa kwake na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa awamu mbili za TASAF zilizotangulia na akaagiza awamu ya Tatu ya TASAF inayotekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini iendeleze yale mazuri yote yaliyopatikana pamoja na kuongeza ubunifu na ufanisi katika kutekeleza Mpango huu.

TASAF III ina sehemu Kuu **Nne**:

1) Mpango wa kunusuru kaya maskini, ambao unatoa ruzuku kwa kaya maskini sana hususan zenye wajawazito na watoto ili ziweze kupata huduma za elimu na afya. Pia kutoa ajira kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi wakati wa majanga mbalimbali kwa mfano ukame, mafuriko n.k.
2) Kuongeza kipato kwa kaya maskini kupitia uwekaji akiba na shughuli za kiuchumi ili kuboresha maisha.
3) Kujenga na kuboresha miundo mbinu inayolenga sekta za **elimu**, **afya** na **maji**.
4) Kujenga uwezo katika ngazi zote za utekelezaji.

TASAF III itatekelezwa kwa miaka kumi katika Awamu mbili za miaka mitano kila Awamu.

- Mpango unalenga kufikia Kaya zaidi ya milioni moja ambazo zinaishi katika hali ya umaskini.
- Utekelezaji wa Mpango unahitaji uwekezaji mkubwa kwenye mifumo na kujenga uwezo katika ngazi zote.

- ❖ Mpango utatekelezwa kwa kuanza na maeneo machache na kuongeza maeneo zaidi kadiri uwezo unavyojengeka na utekelezaji unavyoendelea.

2.0UTAMBUZI, UHAKIKI NA UANDIKISHA JI NA MALIPO

2.1 Zoezi la Utambuzi wa Kaya Maskini lilivyofanyika katika Mkoa

Kaya maskini sana kwa ajili ya kunufaika na Mpango zilitambuliwa na Jamii yenyewe kwa kuzingatia sifa zilizowekwa. Utambuzi ulifanyika kwa utaratibu uliowekwa na viongozi wa TASAF Makao makuu. Zoezi hili lilianza kutekelezwa kwa kuanza kufanya shughuli za Utambuzi wa kaya Maskini, uandikishaji na baadaye utoaji wa Ruzuku (Uhawilishaji).

- Wawezeshaji Ngazi ya Halmashauri walikutana na Halmashauri ya Vijiji walitambulisha Mpango na Kueleza idadi ya Walengwa wanaotakiwa katika kijiji husika.
- Wawezeshaji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji walikutana na mikutano mikuu ya vijiji, wakautambulisha Mpango, kueleza idadi ya walengwa wanaohitajika, kupata wakusanya taarifa kutoka kwenye kila kitongoji.

- Wakusanya taarifa waliorodhesha majina ya kaya maskini sana kwenye vitongoji vyao kufuatana na idadi inayohitajika kwa kuzingatia sifa za kaya maskini walizopewa:-

2.2 SIFA ZA KAYA MASKINI ZILIZOTUMIKA

(i) Ina kipato cha chini sana na si cha uhakika ukilinganisha na kaya zingine kijijini/mtaa.

(ii) Haiwezi kumudu au haina uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku;
Hii ina maana kwamba kaya ya namna hii haiwezi kupata milo mitatu kwa siku.

(iii) Inaishi kwenye makazi duni sana;
Kaya hii inaishi katika makazi duni kupindukia kiasi cha kuhatarisha maisha na afya za wanakaya husika.

(iv) Kaya yenye watoto wenye umri wa kuwa shule lakini hawajaandikishwa au wameacha shule kwa kushindwa kumudu gharama;

- Kaya yenye watoto wanaosoma lakini haiwezi kumudu mahitaji muhimu yanayohitajika shuleni kama vile sare, madaftari, kalamu na michango mingine
- Kaya ambayo ina watoto wanaostahili kuandikishwa shuleni lakini hawajaandikishwa kutokana na ugumu wa maisha katika kaya husika
- Kaya ambayo ina watoto ambao wameacha shule kabla ya muda wa kuhitimu kutokana na ugumu wa maisha katika kaya husika

(v) Ina watoto ambao hawaendi kliniki kupata huduma za Afya.

- Kaya haiwezi kumudu kugharamia mahitaji muhimu ya kumwezesha kumpeleka mtoto kliniki kama vile mavazi ya mama na mtoto au bima ya afya

(vi) Ina watoto wengi

- Kaya yenye watoto wengi ambao haiwezi kumudu kugharamia mahitaji muhimu katika kaya kama vile makazi, malazi, mavazi, chakula, elimu na afya

3.0 MADHUMUNI YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI

- **Kuwezesha kaya maskini sana kuongeza matumizi muhimu kwa njia endelevu**
- **Kuwezesha kuwa na matumizi wakati wa hari (Majanga)**
- **Kuwekeza kwenye rasilimali watu hususani watoto**
- **Kuimarisha shughuli za kuongeza kipato**
- **Kuongeza matumizi ya huduma za jamii**

2.3 Changamoto Katika Utambuzi wa Kaya Maskini

- Dhana potofu kuwa fedha ni za Freemason/Zimelenga Uchaguzi Mkuu
- Baadhi ya mikutano mikuu kupitisha kaya zisizo na sifa,
- Wananchi kuwa na mwitikio mdogo kuhudhuria kwenye mikutano ya maamuzi
- Wananchi kutoamini kuwa Serikali ingeweza ikatoa Ruzuku ya fedha taslimu (kiini macho)
- Waliopitishwa na mikutano mikuu kutotoa taarifa sahihi wakati wanadodoswa.
- Ukosefu wa uadilifu kwa baadhi ya wakusanya taarifa ambao walikuwa wanadodosa taarifa za kaya

3.0 UTOAJI WA RUZUKU KWA WALENGWA (UHAWILISHAJI FEDHA)

Zoezi la malipo lilifuata baada ya zoezi la uhakiki na uandikishaji kukamilika. Malipo ya walengwa hufanyika kila baada ya miezi miwili kwa kufuata kalenda maalum iliyotolewa na TASAF Makao makuu (Master calendar). Malipo haya hufanywa na wananchi wenyewe kwa kutumia Kamati za Usimamizi wa Miradi za Vijiji zilizoundwa na mikutano mikuu ya vijiji.

3.1 AINA ZA RUZUKU NA VIWANGO VITOLEWAVYO KWA WALENGWA.

Mpango una ruzuku za aina mbili ambazo ni Ruzuku ya msingi na Ruzuku inayotegemea kutimiza masharti ya Elimu na Afya.

3.1.1 Ruzuku ya Msingi

Ni ruzuku ambayo haina masharti yoyote na inatolewa kwa kaya iliyomo kwenye Mpango kiasi cha **Shs 10,000** kwa mwezi. Kama kuna mtoto au watoto wenye umri chini ya miaka 18 ambao kwa sababu ya hali zao duni imesababisha wasisome, kaya itaongezwa kiasi cha shilling **4,000/=** kila mwezi.

3.1.2 Ruzuku inayotegemeautimizaji masharti ya Elimu na Afya.

Ruzuku hii inatolewa tu kwa wahusika ambao wameweza kutimiza masharti ya Afya na Elimu kwa kuhudhuria shule ama kliniki kwa kiwango kilichowekwa. Aidha. Kwa muhusika ambaye atashindwa kutimiza masharti ruzuku hii hukatwa moja kwa moja na TASAF Makao Makuu (hailetwi). Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa malipo na makato kwa wasiotimiza masharti.

Jedwali Na. 1 : Viwango vya malipo na makato kwa wasiotimiza masharti ya mpango

Aina ya Mlengwa	**Masharti ya Afya**	**Uhakiki wa Masharti**	**Adhabu (asipotimiza masharti)**
Mtoto mwenye umri wa Miaka 0-2	Kila mwezi kuhudhuria kliniki	Kila baada ya miezi miwili	Makato ya Ruzuku ya **Tshs 4000** kwa kaya
Mtoto mwenye umri wa Miaka 2-5	Kila mwezi kuhudhuria kliniki	Kila baada ya miezi sita	Makato ya Ruzuku ya **Tshs 4000** kwa kaya isiyotimiza masharti
NB: Mtoto chini ya miaka 0-5 Shilingi 4,000/= kila mwezi kwa kuhudhuria kliniki kufuatana na umri na taratibu za wizara ya Afya.			
	Masharti ya Elimu		
Mtoto/Watoto wanaosoma Shule ya Msingi Shilingi 2,000/= kwa mwezi kwa kila mtoto kwa mwezi kwa watoto wasiozidi **4** katika kaya.	Kuhudhuria shuleni kwa 100% ya siku za masomo	Mahudhurio 80% ya siku za masomo	Makato ya Ruzuku ya **Tshs 2000** kwa mtoto asiyetimiza
Mtoto/Watoto wanaosoma shule ya sekondari kidato **1-4** shillingi **4,000/** kwa kila mtoto kwa watoto wasiozidi **3** kwa kila mwezi.	Kuhudhuria shuleni kwa 100% ya siku za masomo	Mahudhurio 80% ya siku za masomo	Makato ya Ruzuku ya **Tshs 4000** kwa mtoto asiyetimiza
Mtoto/watoto wanaosoma shule ya sekondari kidato cha **5-6** shilingi **6,000**/= kwa kila mtoto kwa watoto wasiozidi 2 kila mwezi.	Kuhudhuria shuleni kwa 100% ya siku za masomo	Mahudhurio 80% ya siku za masomo	Makato ya Ruzuku ya **Tshs 6000** kwa mtoto asiyetimiza

- Utimizaji wa masharti ni mhimu ili kupata uhakika wa kufikiwa kwa lengo la kujenga raslimali na kIsha kupunguza umaskini.

- Uhakiki wa utimizaji masharti ndiyo njia halisi ya kufanya ruzuku kuwa sehemu ya motisha kwa maendeleo ya jamii.

7.0 MPANGO WA KUJENGA UWEZO WA KUJIKIMU

- ❑ Kuhamasisha walengwa kuweka akiba, kutekeleza shughuli za kiuchumi na kujiunga katika vikundi.
- ❑ Kuvipatia vikundi zana muhimu kwa ajili ya kuweka akiba.
- ❑ Kutoa mafunzo na kujenga uwezo kulingana na mahitaji ya vikundi.
- ❑ Kuandaa vikundi na kuviunganisha na taasisi mbalimbali za fedha ili kuweza kukuza uwezo wao wa kifedha.

8.0 MIRADI YA KUTOA AJIRA YA MUDA

Miradi ya kutoa ajira za muda ni sehemu mojawapo ya Mpango wa kunusuru kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi.

Madhumuni ya miradi ya kutoa ajira za muda ni kutoa fursa zifuatazo:

- ➢ Kutoa ajira ya muda kwa walengwa ili kuongeza kipato na matumizi kwenye Kaya,
- ➢ Kupata miundombinu katika jamii, na
- ➢ Kuongeza ujuzi kwa walengwa.

8.1 KANUNI ZA MIRADI YA AJIRA ZA MUDA

1. Matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi (Labour Based Technology)
2. Miradi itokane na hitaji la jamii
3. Miradi itatekelezwa kwa kipindi cha hari
4. Ujira utalipwa siku 15 za kufanya kazi kwa mwezi kwa muda wa miezi 4 kwa mwaka (siku 60).

5. Kaya zilizoorodheshwa katika masijala ya walengwa ndizo zitakazotekeleza miradi ya ujenzi isipokuwa pale panapotokea majanga.
6. Mradi utakaotekelezwa usiwe mbali na makazi ya walengwa.
7. Miradi izingatie uwepo wa shughuli nyingine zilizopewa kipaumbele katika jamii (kwa mfano miundo mbinu ya umwagiliaji iendane na mahitaji ya kilimo ya eneo husika)
8. Akina mama watapewa kipaumbele katika kupanga na kutekeleza miradi.
9. Mradi ulenge kupatikana kwa miundo mbinu itakayoleta manufaa kwa jamii.
10. Kuzingatia sera ya kulinda mazingira, uhamishwaji wa makazi na kulinda wenyeji asilia.

8.2 AINA YA MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

- **Hifadhi ya udongo na maji .**
  - Kwa mfano:- Makinga maji,
- **Utengenezaji wa vitalu vya miti na matunda mbali mbali**
  - Kwa mfano:- Kuanzisha vitalu vya miche ya miti na majani .
- **Kuhifadhi maeneo yaliyoharibiwa na binadamu au wanyama**
- **Kilimo mseto - Agro-Forestry**

Kwa mfano:- Kuhifadhi ardhi na kuchanganya Miti na Mazao ya Kilimo, kunde, n.k

- **Miradi midogo ya umwagiliaji**
  - Kwa mfano:- Umwagiliaji kwa njia ya mifereji,Visima vilivyochimbwa kwa mkono, Uvunaji wa maji ya Mvua, Ujenzi wa Malambo n.k
- **Barabara za jamii**

- Kwa mfano:- Ujenzi wa madaraja ya waenda kwa miguu, karavati,Usafishaji wa mitaro n.k

8.3 MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

Aina ya miradi itakayotekelezwa:

- Ujenzi/Ukarabati wa madarasa ya shule za msingi na sekondari, nyumba za walimu, vyoo, maji, ofisi za walimu, maktaba, maabara na mabweni
- Ujenzi/Ukarabati wa miundo mbinu ya afya (zahanati, huduma za mama na mtoto, vyoo, vichomeo taka na maji
- Ujenzi wa miundombinu ya maji

3.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI MKOANI

Mkoa wa Simiyu umeanza kutekeleza zoezi la uhawilishaji fedha kwa kaya maskini tangu mwezi Julai, 2015. Aidha, tangu kuanza kwa zoezi la uhawilishaji hadi malipo yanayoishia Oktoba, 2016 jumla ya shilingi **14,777,004,545.45** zimepokelewa kwa mchanganuo ufuatao:-

- Fedha kwa ajili ya Walengwa Tsh **14,562,272,000.00**
- Fedha kwa ajili ya usimamizi wa Mpango ngazi ya Wilaya **Tsh 1,406,583,090.00**
- Fedha kwa ajili ya usimamizi wa Mpango ngazi ya kijiji **Tsh 248,220,545.45**
- Fedha kwa ajili ya usimamizi wa Mpango ngazi ya Kata **Tsh. 165,480,363.64**
- Fedha kwa ajili ya usimamizi wa Mpango ngazi ya Mkoa **Tsh 165,480,363.64**

Katika mchanganuo huo jumla ya **Tshs 16,382,556,000.00** zilipelekwa katika maeneo ya utekelezaji **Tshs 165,480,363.64** zilipelekwa ngazi ya Mkoa kwa

ajili ya ufuatiliaji wa Mpango. Jedwali lifuatalo linaonesha fedha zilizopelekwa kwa kila Halmashauri.

Uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Desemba, 2016

Eneo	Kiasi Idhinishwa	Pelekwa kwa walengwa+1.5%	Usimamizi na ufuatiliaji Mkoa (1%)	Uwezeshaji na ufuatiliaji wilaya (9.5%)	
				LGA - 8.5%	Ward - 1%
Bariadi	5,259,590,909.09	4,707,333,863.64	52,595,909.09	447,065,227.27	52,595,909.09
Busega	1,604,436,363.64	1,435,970,545.45	16,044,363.64	136,377,090.91	16,044,363.64
Itilima	2,581,690,909.09	2,310,613,363.64	25,816,909.09	219,443,727.27	25,816,909.09
Maswa	4,832,831,818.18	4,325,384,477.27	48,328,318.18	410,790,704.55	48,328,318.18
Meatu	2,269,486,363.64	2,031,190,295.45	22,694,863.64	192,906,340.91	22,694,863.64
Jumla	**16,548,036,363.64**	**14,810,492,545.45**	**165,480,363.64**	**1,406,583,090.91**	**165,480,363.64**

TASAF- Payment Windows

Kulingana na jedwali hilo, Wilaya za Itilima, Busega, na Meatu zimepokea fedha kidogo ukilinganisha na Wilaya za Maswa na Bariadi kwa sababu ya kuwa na walengwa wachache.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni mojawapo ya Wilaya zitakazotumika katika upimaji wa Matokeo ya Mpango wa kunusuru kaya Maskini ambapo ilianza zoezi la uhawilishaji tangu Mwezi wa Septemba, 2015.

3.1 MANUFAA YA MPANGO

Mpango wa kunusuru kaya Maskini umeweza kuwa msaada mkubwa kwa kaya ambazo hazijiwezi kiuchumi. Aidha, mpango huu umeweza kufurahiwa na kaya hizi za walengwa na pia wafanyabiashara kutokana na kuongeza mzunguko wa fedha katika eneo la walengwa. Manufaa ambayo yamepatikana katika Mpango huu ni kama ifuatavyo:-

i. Wanufaika wameweza kujikimu kwa kutumia fedha wanazopata kwa kununua chakula na sare kwa ajili ya watoto wa shule.

ii. Watoto ambao walikuwa wameacha shule kwa kukosa sare na mahitaji mengine muhimu ya shule wameweza kurudi na kuendelea na masomo.

iii. Walengwa wamejiunga katika Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kuweza kufaidika na matibabu wao pamoja na familia zao. Kwa mfano Wilaya ya Maswa walengwa **5,132** hadi Agosti 2016 wamejiunga na mfuko wa Afya CHF na Bariadi kaya **2,549,Meatu 1,096 na Busega 2,574**.

iv. Mpango umesaidia kuongeza uandikishaji wa Wanafunzi wa awali na darasa la kwanza kutokana na hitaji la utimizaji wa masharti ya mpango

v. Mpango umeweza kuongeza mahudhurio ya watoto kliniki na shule.

vi. Kaya za Walengwa zimeweza kuaminika na kukopesheka kwa wafanyabiashara kutokana na kuwa na chanzo cha mapato kinachoaminika. Mnufaika wa kijiji cha Mwandoya Chimaguli aliweza kukopeshwa mifuko 20 ya saruji.

vii. Mpango umewezesha baadhi ya kaya kuwa na vitega uchumi/miradi midogomidogo kama ambavyo imeonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

a) Wilaya ya Bariadi

Walengwa na Shughuli walizofanya

Na	Kijiji	Jina la Mlengwa	Shughuli alizofanya
1.	Masewa	Paulina Halawa	▪ Ana Mgahawa ▪ Amejenga nyumba ya tofali za saruji na imepauliwa
2.	Masewa	Minza L. Kabadi	▪ Ana Mgahawa ▪ Amejenga nyumba ya tofali za saruji na imepauliwa
3.	Sakwe	Esta Subi Kulwa	▪ Amenunua mbuzi na sasa wamezaana na kufikia **12**
4.	Sakwe	Leah Nyenyeki Gana	▪ Amejenga nyumba yenye bati **20**
5.	Malambo	Kulabya M. Misambo	▪ Amejenga nyumba yenye vyumba **2** na sebule na imefikia hatua ya lenta.

			▪ Amenunua bata **5** na kuku **1**
6.	Sapiwi	Faustine Simbila	▪ Ng'ombe mmoja, Bata 4 na Kuku 3

b) Wilaya ya Maswa

Walengwa na Shughuli walizofanya

Na	Kijiji	Jina la Mlengwa	Alichofanya
1.	Igwata	Elizabeth N. Nghobo	Amenunua Ng'ombe 1
2.	Igwata	Kafuleni N. Mabula	Amenunua Bati 10
3.	Ngh'ami	Sado Deshi Shaban	Amenunua Mbuzi 7
4.	Zebeya	Luja Masanja	Amenunua Mabati 12
5.	Igumangobo	Elizabeth Mandago	Amenunua Mbuzi 4, mabati 16
6.	Bukangilija	Yunge Charles	Amelima mpunga na kuvuna magunia 15

c) Wilaya ya Meatu

Walengwa na Shughuli walizofanya

Na	Kijiji	Jina la Mlengwa	Alichofanya/nunua/wekeza
1.	Malwilo Mnadani	Mbuke Jongela	Amenunua Mabati 8
2.	Itongolyangamba	Silya T.Machibya	Amenunua shamba la ekari 2
3.	Lubiga	Sayi Charles	Amenunua Mbuzi 2 na Baiskeli 1
4.	Semu	Dilu S.Kidinya	Amenunua Mbuzi 5
5.	Semu	Ng'walu Ntinjiwa	Mgahawa
6.	Mwandoya	Chimaguli	• Amejenga nyumba ya matofali ya saruji vyumba 4 iko hatua ya upauaji • Anafanya biashara ya dagaa na samaki

3.2 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI.

Katika zoezi la uhawilishaji zifuatazo ni baadhi ya changamoto zilizojitokeza:-

i. Baadhi ya walengwa walioandikishwa na kuhakikiwa majina yao kutoonekana kwenye orodha ya malipo licha ya kuwa na vitambulisho

vya walengwa. Mfano Halmashauri ya Wilaya ya Maswa Walengwa **23** ambao wana vitambulisho vya mpango majina yao kutokuwepo katika orodha ya malipo toka kuanza kwa malipo Julai **2015** hadi Septemba **2016**

ii. Kutofautiana kwa majina ya wanafunzi wanaosoma shule za msingi, sekondari na wanaohudhuria kliniki na majina yaliyopo TASAF Makao Makuu

iii. Baadhi ya Vijiji vilipitisha walengwa ambao hawana sifa za kuwemo katika Mpango kutokana na wanasiasa pamoja na watu mashuhuri kutumia vibaya nyadhifa zao.

iv. Baadhi ya wanakamati wamekuwa si waaminifu kwani wanadiriki kuiba fedha za wanufaika (Somanda, Kilulu n.k)

v. Wanakamati wamekuwa wakitumia muda mwingi Benki wakati wa zoezi la kuchukua fedha za Walengwa hasa Wilaya za Bariadi, Itilima na Busega kutokana na kuhudumia Wilaya 2 kwa wakati mmoja.

vi. Baadhi ya walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini kushindwa kutimiza masharti japo wamekuwa wakisisitizwa kufanya hivyo.

vii. Walengwa waliobainika kuwa wana uwezo na waliingizwa kimakosa na mikutano mikuu ya vijiji wamekaidi kurejesha fedha walizopokea.

viii. Walengwa wengi walioko katika mpango wa kunusuru kaya maskini wanahama kwenda mikoa mingine na baadhi yao hawatoi taarifa kwenye uongozi wa serikali ya kijiji.

ix. Baadhi ya Vijiji, wananchi wanaogopa kuwataja walengwa ambao hawana sifa za kuwemo katika mpango.

3.3 MAPENDEKEZO YA UTATUZI

i. Majina ya walengwa wenye vitambulisho lakini hawapo katika orodha ya malipo yalishawasilishwa TASAF makao makuu ili yaingizwe katika orodha ya malipo.

ii. Kamati za vijiji zinazohusika na mradi wameshauriwa kuwajazia fomu za mabadiriko ya taarifa ili majina yaliyopo katika fomu yafanane na yaliyopo katika usajili wa shule

iii. Jumla ya kaya za Walengwa **1747** zisizo na sifa zimeondolewa katika Mpango.

iv. Kwa maeneo ambayo yanakuwa hayawezi kupitika kwa gari, walengwa wamekuwa wakishauriwa kusogea katika vijiji vya jirani ili kupokea ruzuku yao

v. CMCs ambazo zimeonekana kutokuwa waaminifu zimevunjwa.

vi. Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Itilima na Busega wameshauriwa kuongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB ili wafungue matawi katika maeneo yao.